


# Jicho kwa ajili ya huduma ya watoto

Sikumoja bwana yangu Dwight na mimi tulikuwa kwa ziara kubwa na tulikuwa na ziara njema na gari,wakati Mungu mara moja alitufungua macho kwa umuhimu wa wizara ya watoto.tulikuwa tunaongea kuhusu mipango ya wizara na tukiomba pamoja.huku tukiomba Mungu alinipea ono.

Niliona umati mkubwa wa watu wakikimbia chini kwenye mtaa mpana.ilikuwa inafanana na mbio za masafa marefu zikiwa na maelfu na maelfu ya wakimbiaji.watu wote walikuwa wanakimbia pamoja chini kwenye mtaa.hakuna aliyekuwa anatambua yakuwa mbele yao kulikuwa ndio mwisho wa mtaa na kulikuwa na mwanguko mkubwa.watu waliendelea kukimbia hadi wakafika kwenye mwanguko ambapo waliingia hadi chini.kwenye ardhi palikuwa na rundo la watu walio umia.

## Kulikuwa na kundi la watu waliokuwa wakikimbia chini kusaidia watu walioumia.

niliona hema zilizowekwa kama hospitali ndogo na ciniki za afya.madaktari na wauguzi walileta watu kwa hema na kuwasaidia.wengine walikuwa na miguu zilizovunjika,wengine walikuwa wanahitaji bendeji na wengine walikufa.

Mungu alinionyesha yakuwa hema tofauti zilionyesha madhehebu za dunia.madaktari walikuwa wachungaji,na wale wote walikuwa wanasaidia walioumia ni wale walioko kwenye wizara.kulikuwa na wakati ambapo watu watatu walikuwa wanajaribu kusaidia mtu 1 aliyekuwa ameumia,na sasa dhehebu mbalimbali zilikuwa zinangengana ataenda kwa hema ya akina nani.


Watu ambao walikuwa wanakimbia kwenye mtaa ju walikuwa wana wakilisha watoto.mungu alinionyesha yakuwa ni watu kadhaa tu ndio walikuwa wanasaidia watoto na kuwaonya ju ya mwanguko ambao kila mtu alikuwa anaanguka.wizara yote ilikuwa inaenda chini ya jabali(cliff),kusaidia wale waliokuwa wameumia.Lakini wengi ndio waliokufa,na vifo hivyo zinge zuiwa,bila kutaja kuzuia uchungu wote.

Mifupa iliyo vunjika na bendeji zilionyesha uchungu ambao watu walikuwa wamepata kabla ya kujua yesu na akabadilisha maisha yao.uchungu wa taliki,uchungu wa kuiba duka na kuenda jela,uchungu wa

kuoa asiye sahihi,na uchungu wa kupatikana kwenye dhambi tofauti.kulikuwa na watu wengi kwenye wizara ambao walikuwa wanasaidia watu waliokuwa na shida zao,lakini kulikuwa na watu wachache waliokuwa wana saidia watoto kabla ya wao kuanguka.

## Wizara huko chini ilikuwa inafurahi kwani ungepata mtu aliyekuwa karibu kufa,na ungempee CPR.kwa muda wa dakika chache,utakuwa umeokoa maisha ya mtu!

gari la wagonjwa zingefika huku vingora zikilia kwa sauti na kila mtu angeona kile ambacho ulikuwa unafanya ukiwaweka na kuwapeleka kwenye hema za madhehebu.lakini juu,kufanya kazi na watoto,wakati ulisimamisha mtu kutoka kwanguka toka kwa jabali.hakukuwa na mbwembwe.hakukuwa na kelele na hakna mtu aliona kitu cha kupendeza.kulikuwa na mtu ambaye aliacha kukimbia na wengine na akaacha kabla ya kuanguka.



Kwahivyo,Dwight na mimi tulihisi nikama macho yetu yalikuwa yamefunguliwa kwa wizara ya watoto.haikuwa wizara kwa watoto.ilikuwa wizara ya binadamu,roho mzima na nafsi.wizara ya watoto inasimamisha watu toka kukimbia pamoja na umati kwenye maafa ambayo yanaeza zuiwa.ile kiyu ndogo na watoto ni mili yao na vibeti zao.huwa hawatoi kifungu cha kumi,na wanakaa wafupi sana.lakini nikama sifongo,kuchukua maelezo mengi,na kusoma jinsi ya “kukimbia”kwenye maisha hii.

Dwight na mimi tuliamua kuacha hema zetu huko chini na kukwea juu na kuanza kazi ya KUSIMAMISHA watu kutoka kuanguka chini la jabali.kutoka hapo watu wachache wanafanya kazi kwenye wizara ya watoto,ilionekana muhimu kulenga wale husaidia.kazi yetu nikusaidia wale walio juu na kufanya kazi kuwaweka hapo juu.
Kwa miaka 10 iliyopita ambayo nimekuwa misionari mexico,nimepata yakuwa 90% ya wafanyikazi hawapangi kukaa kwenye wizara ya watoto.wako hapo hadi wapewe nafasi bora Zaidi kwenye Kanisa zao.naelewa kabisa kwani nilifanya hivyo pia.niliishia kutumika wizara ya watoto kwa miaka 18,lakini sikuwa napanga kukaa hapo!nilianza hapo kwa sababu ilikuwa mahali pa kutumikia ndani ya kanisa.niliishi kudhani nitahamia kwenye wizara ya kina mama na kisha kuwa bibi ya mchungaji.nilifurai wakati tulikuwa wamisionari,kwani nilikuwa juu Zaidi ya ngazi la jumuia ya wakristo.

## Lakini,sikuwai fikiria kurudi kwenye wizara ya watoto.

Kwenye siku ya tukio kwenye gari,huku tukiwa kwenye safari,Dwight na mimi tulihisi mwito wa Mungu kwenda kwenye wizra ya watoto.haikuwa kuitwa pekee bali tulihisi nikama Mungu alituonyesha kufikiria kwake.lazima kuna mtu angeamka aende kwenye jabali juu na kuonya watu kuhusu kuanguka,ilikuwa bora Zaidi kusimamisha watu kutoka kuanguka kuliko kutengeneza uharibifu chini.
Natumai yakuwa na ono hili,Mungu amefungua macho yako kwenye mwito wa wizara ya watoto.

Haina lolote na kufunza kwa ukweli.inahusisha kufanya kazi na nafsi za ukweli kabla zianguke kwa dhambi ambazo zitazamisha maisha yao.

**Kwenye wizara ya watoto,tunahitaji wachungaji,makasisi,walimu,wapishi,waandaji,mameneja wa kampeni kwenye kitabu cha uso(facebook),wataalam wa sauti,waimbaji,wachoraji, na Zaidi.kila kitu mwili wa yesu uko nayo,wizara ya watoto inahitaji.**

hatutafuti walimu pekee.tunahitaji  usaidizi wa kila mtu.tunahitaji watu kuwafungua macho,na kutumikia kwenye idara ya upendo kwenye wizara ya watoto.tutachukua usaidizi toka kwa watu wasio wa kudumu kwa sababu tunahitaji  usaidizi kabisa.lakini TUNAHITAJI watu wazima ambao wako na nia kwenye wizara ya watoto,na wako na nia ya kusaidia nafsi za ukweli KABLA ya kuanguka toka kwa jabali!

Vision for Children's Ministry Swahili

20132

www.ChildrenAreImportant.com
info@childrenareimportant.com
We are located in Mexico.
DK Editorial Pro-Visión A.C.

Watoto ni wa muhimu